# BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

**BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA PILI**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 6 Juni, 2016.**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2016/2017.

**Mwenyekiti, Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari:**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari kuhusu Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2016/2017.

## II. MASWALI:

### OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:

78. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Ukosefu wa ajira ni miongoni mwa Changamoto za nchi zinazoendelea ikiwemo hapa kwetu Zanzibar ambapo hali hii inapelekea vijana wengi kuzurura mitaani baada ya kumaliza masomo wakiwemo wale wanaofaulu vizuri.

a) Ni nini hasa sababu za ukosefu wa ajira hapa nchini kwetu.

b) Serikali imejipanga vipi kukabiliana na tatizo hili.

c) Kwa nini Serikali imekuwa ikiwapatia mikataba ya mara kwa mara wafanyakazi wanaomaliza muda wao wa utumishi kuendelea kuwemo katika ajira ya Serikali wakati vijana wengi na wenye ujuzi wanazurura mitaani.

### WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

58. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Chukwani) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa muda mrefu kumekuwa na usumbufu kwa wanafunzi wa Buyu na Shakani kukosa skuli za karibu na kupata usumbufu wa kufuata elimu masafa ya mbali. Aidha, zipo taarifa kuwa kiwanja cha ujenzi wa skuli ya Buyu pia kimeuzwa.

a) Serikali ina mpango gani kujenga skuli maeneo ya Buyu na Shakani ili kuwapunguzia shida watoto ambao wanafuata huduma hiyo masafa ya mbali.

b) Je kama kiwanja kilichokusudiwa kujengwa skuli Buyu kimeuzwa, Serikali inayo mpango kukirejesha kiwanja hicho au kutafuta eneo jengine na kujenga.

**WIZARA YA ARDHI, MAJI, NISHATI NA MAZINGIRA:**

63. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Tangu kuundwa kwa Kamisheni ya Ardhi kumekuwa na shida na mateso wanayopata wananchi kwa kufuatilia "*lease*" zao ambazo inachukua muda mrefu kuzipata.

Je, ni sababu gani zinazochelewesha kupatikana "lease" kwa wakati.

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:**

108. MHESHIMIWA YUSSUF HASSAN IDDI (Jimbo la Fuoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Wahasibu Wakuu wa VOTE, Wasaidizi Wahasibu Wakuu wa VOTE na Wakaguzi Wakuu wa ndani wa VOTE, wanafanya majukumu yao ya kiutendaji sawia katika taasisi moja lakini wanapishana sana kimaslahi.

a) Je, kwanini Wahasibu Wakuu wa VOTE wanapishana sana kimaslahi (mshahara) na Wasaidizi wao.

b) Je, kwanini Wahasibu Wakuu wa VOTE wanapishana sana kimaslahi na Wakaguzi Wakuu wa ndani wa VOTE hiyo hiyo wakati wapo ngazi moja ya uongozi.

c) Je, Serikali haioni mpishano huo mkubwa uliopo wa mshahara unavunja moyo na kupunguza ari na ufanisi katika kazi.

**WIZARA YA AFYA:**

24. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wananchi walipata faraja sana baada ya Serikali ya Awamu wa Saba kuleta vipimo vya kisasa, lakini upatikanaji wa kipimo cha CT SCAN haupo katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa muda mrefu na kuleta usumbufu mkubwa sana kwa wananchi masikini wanaoshindwa kupata huduma katika hospitali binafsi. Kwa kuwa kipimo hichi ni muhimu sana kwa watu wanaopata ajali barabarani na watu wenye magonjwa makubwa yanayohitaji uchunguzi wa kina.

a) Je Serikali haioni kuwa kukosekana kwa kipimo hicho inachangia vifo kwa watu wanaohitaji huduma za uchunguzi wa kipimo hicho.

b) Iko wapi faida baada ya Serikali kutangaza huduma hiyo ipatikane bure kwa wananchi wakati huduma hiyo haipatikani.

c) Kwanini katika hospitali binafsi vipimo hivi vinasimamiwa vizuri mashine zake na zinapoharibika hutengenezwa kwa wakati; wao wanaweza vipi na kwa nini Serikali inashindwa na hatua gani zimechukuliwa kwa watendaji dhamana.

**WIZARA YA UJENZI, MAWASILIANO NA USAFIRISHAJI:**

74. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Tunaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutengeneza barabara nyengine inayoelekea Wesha kutokea Tibirinzi ambayo pia ina daraja la enzi pale Pondeani, badala ya ile ya kupitia katika daraja la Tingatinga ambalo limekatika kwa maji kwa muda mrefu sasa.

a) Kwa kuwa tunafahamu umuhimu wa eneo la Wesha ukizingatia kwamba ni sehemu muhimu yenye Mitambo ya umeme na vituo vya mafuta, Je Serikali haioni umuhimu wa kulifanyia matengenezo daraja la Tinga

Tinga kabla ya lile la Pondeani halijaanza kuleta madhara.

b) Kama Serikali haijawa na nafasi ya kulitengeneza daraja hili la Tinga Tinga, kwa nini isifikirie kujenga angalau Daraja la vyuma ili kunusuru maisha ya watumiaji wa daraja hilo hivi sasa.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2016/2017.

**Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo:**

Kwamba Baraza hili liingie katika Kamati ili kujadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa Mwaka 2016/2017.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**6 Juni, 2016.** **KATIBU WA BARAZA**